TANGAZO LA SERIKALI Na. 1041 la tarehe 18/12/2020

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

## SHERIA NDOGO ZA USHURU WA STENDI NA MAEGESHO YA MAGARI ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi na Maegesho ya Magari za Halmashauri ya Wilaya ya Siha za mwaka, 2020.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo cha moto au chombo cho chote kinachotumika kusafirishia bidhaa, abiria au mizigo.

"Halmashauri" maana yake Halmashauri ya Wilaya ya Siha;

"kupiga debe" maana yake ni kushawishi abiria kusafiri kwa kutumia chombo fulani cha usafiri kwa kumshika au kumsongasonga au kushika mzigo wa abiria huyo.

"stendi" maana yake ni eneo maalum

lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au kupakia na kushusha mizigo.

"Stendi ya Halmashauri" maana yake ni stendi kuu ya magari ya abiria ndani ya Wilaya;

"maegesho ya magari" maana yake ni eneo ndani ya stendi ya Halmashauri linalotumika kuegesha au kulaza chombo cha usafiri.

"muda wa kawaida" maana yake ni kuanzia saa 12.00 alfajiri mpaka saa 2:00 usiku;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri au Afisa ye yote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru wa stendi" maana yake ni ushuru unaotozwa na Halmashauri kwa chombo cha usafiri kinachopita, kinachopakia au kushusha abiria, au kupakia na kushusha mizigo katika eneo la stendi;

"vituo vya njiani" maana yake ni vituo vyote vilivyopo pembeni ya barabara vinavyotumika kupakia na kushusha abiria ambavyo siyo stendi;

"Yadi" maana yake ni eneo lililotengwa kwa ajili ya kuhifadhi vyombo vya usafiri.

Ushuru wa Stendi

4. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa stendi kwa vyombo vyote vya usafiri kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kila mtu au chombo cha usafiri kinachoingia katika eneo la stendi kinatakiwa kulipiwa ushuru wa stendi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kinapoingia katika eneo la stendi, au kwa siku au kwa mwezi kadri Halmashauri itakavyoona

inafaa.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) cha Sheria Ndogo hizi, vyombo vya usafiri vinavyomilikiliwa na Serikali, taasisi za kidiplomasia, majeshi, na magari ya kubeba wagonjwa havitatozwa ushuru wa stendi.

Matumizi ya stendi

5. (1) Itakuwa ni wajibu kwa mtu ye yote anayefanya biashara ya kusafirisha abiria, kupakia na kushusha abiria au mizigo yao katika eneo la stendi tu.

(2) Isipokuwa kwa kibali cha Halmashauri muda wa kutumia stendi utakuwa kuanzia saa kumi na mbili (12:00) asubuhi mpaka saa mbili kamili (2:00) usiku.

(3) Magari yote yanayofanya biashara ya usafirishaji ndani ya Halmashauri safari zake zitaanzia kwenye stendi zilizoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi isipokua kwa magari yanayopita kutoka maeneo mengine ya nje ya Halmashauri.

(4) Magari ya abiria hayataruhusiwa kusimama kwa zaidi ya dakika tano katika vituo vya njiani.

(5) Gari la abiria au gari la mizigo halitaruhusiwa kukaa katika eneo la stendi kwa muda unaozidi masaa mawili.

(6) Halmashauri itatenga eneo maalum ndani ya eneo la stendi kwa ajili ya kupakia au kushusha mizigo.

Biashara ndogondogo

6. (1) Wafanyabiashara wa biashara ndogondogo katika eneo la stendi watatakiwa kujisajili kwa msimamizi mkuu wa stendi na kupatiwa vitambulisho.

(2) Itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yote kupiga debe au kufanya jambo lo lote ambalo ni

kinyume na matumizi ya kawaida ya stendi.

Uanzishaji wa Stendi

7. (1) Halmashauri itaanzisha stendi itakayotumika kupakia au kushusha abiria na mizigo.

(2) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1), Halmashauri inaweza kutumia stendi zake kama maegesho ya magari au sehemu ya kulaza magari ya watu binafsi kadri itakavyoona inafaa.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri inaweza kuanzisha stendi ndogo katika maeneo ya vijiji au miji midogo kadri Halmashauri itakavyoona inafaa.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

8. (1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kukamata na kuondoa chombo cha usafiri ambacho kitapakia au kushusha abiria nje ya eneo la stendi au mmiliki au dereva wa chombo hicho atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Chombo cha usafiri kilichokamatwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (1) kitaondolewa na kuhifadhiwa kwenye Yadi ya Halmashauri au sehemu yo yote kama itakavyoamriwa na Mkurugenzi.

(3) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuuza chombo kilichokamatwa baada ya kupata idhini ya Mahakama endapo mmiliki wa chombo hicho atashindwa kulipa gharama za uangalizi pamoja na gharama za kukamata ndani ya siku 14 tangu tarehe ya kukamatwa.

(4) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa kwenye kifungu kidogo cha (3) Halmashauri kabla ya kuuza chombo kilichokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya maandishi kwa umma juu ya kusudio la kuuza chombo hicho.

(5) Halmashauri haitawajibika na hasara yo yote na kwa namna yo yote ile itakayotokea wakati wa

kukamata au kushikilia mali iliyokamatwa isipokuwa pale itakapobainika kuwa Halmashauri ilitumia mamlaka yake kinyume na sheria.

Makosa

9. Itakuwa ni kosa kwa mtu ye yote endapo:-

(a) atakataa au atashindwa kulipa ushuru wa stendi;

(b) atamshawishi mtu yeyote au kundi la watu kukataa kulipa ushuru wa stendi;

(c) atapakia au atashusha abiria au mizigo katika eneo ambalo siyo stendi au eneo lililotengwa kwa ajili hiyo;

(d) atapiga debe katika eneo la stendi;

(e) atafanya matengenezo au kuosha gari katika eneo la stendi;

(f) atalaza gari lake au chombo kingine cha usafiri katika eneo la stendi;

(g) atauza chakula au vinywaji au bidhaa nyingine bila kusajiliwa;

(h) ataanzisha stendi kinyume cha sheria.

Adhabu

1 Mtu ye yote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

Kufililisha kosa

1 Bila ya kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi

atakuwa na madaraka ya kufililisha kosa kwa kumtaka mtu aliyekiri kufanya kosa chini ya

Sheria Ndogo hizi kulipa kiasi cha shilingi laki mbili na kujaza fomu iliyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA

USHURU WA STENDI (VYOMBO VYA KUSAFIRISHA ABIRIA)

| *Na* | *Aina ya Chombo* | *Ushuru Tshs Muda wa kawaida* | *Idadi* |
|---|---|---|---|
| 1 | Basi lenye uwezo abiria 5-15 | 500/= | Kila inapotoka |
| 2 | Basi lenye uwezo wa abiria 16-25 | 1000/= | Kila inapotoka |
| 3 | Basi kubwa zaidi ya abiria 26-35 | 1000/= | Kila inapotoka |
| 4 | Basi kubwa lenye uwezo wa abiria zaidi ya 35 | 2000/= | Kila linapotoka |
| 5 | Tax | 500/= | Kila inapotoka |
| 6 | Pikipiki ya magurudumu mawili | 200/= | Kila inapotoka |
| 7 | Pikipiki ya magurudumu matatu | 300/= | Kila inapotoka |
| 8 | Noah | 500/= | Kila inapotoka |
| 9 | Gari lo lote dogo lisilotajwa hapo juu | 700/= | Kwa inapotoka |

SEHEMU YA PILI

USHURU WA STENDI (KUEGESHA AU KULAZA CHOMBO CHA USAFIRI)

| *Na* | *Aina ya Chombo* | *Ushuru Tshs Muda wa kawaida* |
|---|---|---|
| 1 | Basi lenye uwezo abiria 5-15 | 1,000/= |
| 2 | Basi lenye uwezo wa abiria 16-25 | 1,500/= |

| | | |
|---|---|---|
| 3 | Basi kubwa zaidi ya abiria 26-35 | 2,000/= |
| 4 | Tax | 1,000/= |
| 5 | Pikipiki ya magurudumu mawili | 300/= |
| 6 | Pikipiki ya magurudumu matatu | 500/= |
| 7 | Noah | 800/= |
| 8 | Gari lolote dogo lisilotajwa hapo juu | 700/= |

SEHEMU YA TATU

USHURU WA STENDI (VYOMBO VYA KUSAFIRISHA MIZIGO)

| *Na* | *Aina ya Gari* | *Ushuru Tshs Muda wa Kawaida* | *Ushuru Tshs Usiku* | *Idadi* |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Basi dogo tani 1-5 | 500/= | 1,000/= | kwa siku |
| 2 | Gari dogo abiria 6-10 | 1,000/= | 2,000/= | kwa siku |
| 3 | Gari dogo zaidi 11 | 2,000/= | 3,000/= | kwa siku |
| 4 | Guta | 300/= | - | kwa siku |
| 5 | Ushuru wa mitambo ya ujenzi au kilimo | 5000/= | 10,000/= | Kwa siku |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 11)*

HATI YA KUFILILISHA KOSA

Mimi.......................................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ...............................................ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwamba tarehe..........ya mwezi.......................mwaka...........................nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha..............................cha Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi na maegesho ya magari za Halmashauri ya Wilaya ya Siha za mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, nipo teyari kulipa kiasi cha faini cha shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAEELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo tarehe.....................ya mwezi.........................mwaka......................................

Jina.................................................... Saini...........................................................

Mbele ya:

Jina:................................................Cheo:............................................

Saini......................................................................................................

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa na Mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe 06 mwezi 03 mwaka 2019 na imebandikwa mbele ya:-

NDAKI S. MHULI
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya*
*SIHA*

GODSON J. NGOMUO
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya*
*SIHA*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Novemba, 2020

SELEMANI S. JAFO (MB.)
*WN-OR-TAMISEMI*